**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**650** **HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Year: 2020**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org

TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha sifa ambazo zinaweza kumsaidia Mwalimu wa somo la Haiba na Michezo kutambua kitabu cha kiada.
2. Eleza kwa kifupi namna ambavyo kitabu cha kiongozi cha mwalimu humsaidia mwalimu katika ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.
3. Fafanua kwa kifupi mambo manne yanayotakiwa kuzingatiwa wakati wa kusahihisha kazi za wanafunzi.
4. Ainisha michezo minne inayotumia kanuni na sheria.
5. Eleza kwa kifupi mbinu nne anazoweza kutumia mwalimu wa somo la Haiba na Michezo kuwafundisha wanafunzi walioathirika na kuishi katika mazingira duni.
6. Bainisha kisha kueleza kwa kifupi zana anazoweza kutumia mwalimu wa somo la Haiba na Michezo katika kupima maendeleo ya wanafunzi.
7. Changanua mambo manne yanayoweza kupimwa katika stadi za michezo.
8. Fafanua kwa kifupi mambo anayopaswa kufanya mwalimu katika utekelezaji wa andalio la somo katika hatua ya kukazia maarifa, vitendo vya ufundishaji, vitendo vya ujifunzaji na tafakari.
9. Toa hoja nne na kisha kubainisha uhusiano uliopo kati ya Azimio la kazi na Andalio la Somo katika maandalizi ya ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.
10. Chambua stadi nne anazopaswa kuwa nazo mwalimu wa somo la Haiba na Michezo wakati wa maandalizi ya somo lake.

**SEHEMU B (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Chambua kwa hoja tano, kuhusu mambo yanayochangia kubadilisha tabia na mienendo ya wanafunzi.
12. Fafanua kwa kina stadi tano anazozipata mwanafunzi kwa kushiriki michezo mbalimbali.
13. Thibitisha kwa hoja tano, kuwa Shajara ni zana mtambuka katika utekelezaji wa muhtasari wa somo la Haiba na Michezo.
14. Fafanua umuhimu wa Andalio la Somo katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org